Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA ISHIRINI**

**KIKAO CHA KWANZA – TAREHE 8 JUNI, 2010**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**Wimbo wa Taifa**

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliimba Wimbo wa Taifa)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**TAARIFA YA SPIKA:**

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, katika Mkutano wa Kumi na Tisa (19) wa Bunge hili tulipitisha Miswada sita ya Sheria iitwayo, *The Persons with Disabilities Bill, 2010, The Capital Markets and Securities Ammendments Bill, 2010, The Writen Laws (Misceleneous Ammendments) (No. 2) Bill, 2010, The Livestock Identification, Registration Traceability Bill, 2010, The Grazing-Land and Animal Feed Resources Bill, 2010* na *The Mining Bill, 2010.*

Waheshimiwa Wabunge, kama kawaida kwa kufuata utaratibu wa Katiba, baada ya kupitishwa na Bunge Miswada hiyo ilipita katika hatua zake zote za uchapishaji na kufika kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili atoe kibali chake.

Kwa taarifa hii napenda kuliarifu Bunge hili kwamba Mheshimiwa Rais amekwisha toa kibali chake na sasa Miswada hiyo ni Sheria za nchi. Sheria hizo zinaitwa, *The Persons With Disabilities Act, 2010,* itakuwa ni Sheria Namba Tisa ya Mwaka *2010*, *The Capital Markets and Securities (Amendments) Act, 2010.* Sasa ni Sheria Namba Kumi ya Mwaka *2010*, *The Writen Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Act, 2010,* itakuwa Sheria Namba Kumi na Moja ya Mwaka 2010, *The Livestock Identification Registartion and Traceability Act, 2010,* itakuwa ni Sheria Namba Kumi na Mbili ya Mwaka 2010, *The Grazing-Land and Animal Feed Resources Act, 2010* itakuwa ni Sheria Namba Kumi na Tatu ya Mwaka 2010, *The Mining Act, 2010.* Sasa ni Sheria Namba Kumi na Nne (14) ya Mwaka 2010.

Aidha, Muswada wa *The Electoral Laws (Miscellaneous Amendments)* Bill, 2009 ambao ulipitishwa na Bunge hili katika Mkutano wa Kumi na Nane (18) na ambao ulikuwa haujapata kibali cha Rais, sasa umepata kibali hicho na Muswada huo sasa ni Sheria inayoitwa *The Electoral Laws (Miscellanious Amendments) Act, 2010.* Sasa ni Sheria Namba Saba (7) ya Mwaka 2010, ahsanteni sana. *( Makofi)*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kuwasilisha mezani taarifa ya matoleo ya gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake zilizochapishwa tangu kikao cha mwisho cha Mkutano wa kumi na tisa wa Bunge. Naomba kuwasilisha.

**SPIKA**: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge.

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge kabla sijamwita anayeuliza swali letu la kwanza naomba kuwakaribisha tena Dodoma kwa Mkutano wetu huu wa Ishirini ambao ni Mkutano wa mwisho wa Bunge la tisa, lililoanza Desemba, 2005 mpaka sasa.

Tukishamaliza shughuli hizi basi tunaingia katika Uchaguzi Mkuu Bunge hili au Mkutano huu wa Ishirini ni wa wiki tano tu pamoja na kuwa ni mkutano wa Bajeti. Nashukuru kupata ushirikiano wenu. Haya ni mahitaji ya Katiba tusingeweza kuendelea zaidi ya tarehe iliyopangwa na kushirikishwa kwa Kamati ya Uongozi, na mimi sina uhakika kwamba mna hamu sana tukae Dodoma. Kwa hiyo, mambo yote yamekaa vizuri tu karibuni tushirikiane ili katika wiki tano tuweze kumaliza shughuli zetu, ahsanteni sana.

Waheshimiwa Wabunge, swali la kwanza linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na linaulizwa na Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mbunge wa Busanda.

Na. 1

**Huduma Zinazotolewa na Kituo cha Afya Nyachilulumа**

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA** aliuliza:-

Kituo cha Afya Chilulumа kinahudumia Tarafa ya Butundwe yenye Kata nne zenye jumla ya vijiji 35 lakini hakitoi huduma kubwa za upasuaji hivyo kusababisha vifo vya watu wengi hasa akina Mama wajawazito wakati wa kujifungua ambapo hulazimu kusafirisha kwenda hospitali ya Wilaya ya Geita umbali wa kilomita 50.

Je, Serikali haioni haja ya kupandisha hadhi kituo hicho ili kiweze kutoa huduma bora zaidi kupunguza vifo vya wajawazito?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII (K.n.y. WAZIRI MKUU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kusimama mtu wa kwanza kwa kujibu swali lakini kushukuru pia kwa kunipa nafasi hii.Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kutoa maelezo ya awali kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tarafa ya Butundwe iliyoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita ina Kata 6 na Vijiji 35. Tarafa hii ina vituo vya Afya viwili, yaani Chikobe na Katoro.

Aidha kuna Zahanati 7 za Serikali ambazo ni Bukondo, Kasang'hwa, Chigunga, Nyamwilolelwa, Chibingo, Kaseme na Mukenezi pia kuna Zahati ya Nyasembe ambayo ni ya Madhehebu *Assembly's Inland Church of Tanzania ( AICT).* Zahanati mpya 2 za Serikali zinatarajiwa kufunguliwa hivi karibuni.

Hakuna kituo cha Afya Nyachiluluma bali kuna Kata ya Nyachiluluma yenye kituo cha Afya Chikobe na Zahanati ya Kasang'hwa. Kituo cha Afya Chikobe hakitoi huduma kubwa za upasuaji kwa kuwa hakina uwezo wa kutosha kutoa huduma hiyo. Hakuna nyumba ya upasuaji, hakuna vifaa vya upasuaji, hakuna daktari na hakuna mahitaji mengine muhimu.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha kituo cha Afya Chikobe kilichopo katika Kata ya Nyachiluluma, Serikali imepanga katika mwaka 2010/2011 kukipatia kituo hicho gari la wagonjwa. Aidha kituo cha Afya cha Nzera kitapatiwa huduma za upasuaji mpango wa kukipatia huduma ya upasuaji kituo cha Afya Chikobe utatekelezwa katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, ni azma ya Serikali kuboresha vituo vyote vya Afya ili viweze kutoa huduma bora za Afya zikiwemo upasuaji wa dharula hususan kwa akina mama wajawazito, na kwamba uboreshaji huu utakuwa unafanywa hatua kwa hatua kulingana na upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

**MHE. LOLESIA J.M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa majibu mazuri kutoka kwa Naibu Waziri wa Afya. Kulingana hali halisi katika kituo hiki cha Chikobe akina mama wengi sana wanapata shida wakati wa kujifungua na wengi wanapoteza maisha yao nilikuwa naomba kuuliza kwamba ni lini hasa kituo hiki kitaweza pandishwa hadhi ili kiwe hospitali nashukuru sana kwamba tutapatiwa gari la wagonjwa, lakini bado huduma inahitajika kuboreshwa zaidi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII (K.n.y. WAZIRI MKUU):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lolesia Bukwimba kama ifuatavyo. Kama nilivyosema katika jibu la msingi ni kwamba fedha imetengwa na ni kweli kabisa lakini kwa sababu

haijakidhi hivi hatuwezi kukifanya kituo cha Afya cha kutoa zile huduma lakini nilitaka kusema tu hapa kama mpango wa maendeleo ya Afya ya msingi ulivyo ni kwamba vituo vyote ambavyo viko kwenye vituo vya Afya vinatakiwa zitoe huduma za akina mama ili waweze kutoa huduma za upasuaji.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema ni kwamba kituo hiki hatuwezi kukibadilisha kikawa hospitali kwa sababu tayari hospitali ya Geita ipo.

Nataka kumhakikishia Mheshimiwa kwamba katika mpango wetu wa MMAM tunapotekeleza tunataka kuboresha ifikie hatua ya kuweza kufanya upasuaji na hivyo majengo haya yataongezwa kama nilivyosema kadri pesa itakavyokuwa inaturuhusu.

Na. 2

**Uhaba wa Vyumba vya Wagonjwa Kituo cha Afya Mererani.**

**MHE. DORAH HERIEL MUSHI** aliuliza**:-**

Kwa kuwa Mji mdogo wa Mererani una wakazi wapatao 51,000 na una kituo kimoja cha Afya kilichojengwa kwa ushirikiano wa Serikali na Shirika la *World Vision* pamoja na Michango ya wananchi lakini hakina vyumba vya kulaza wagonjwa na kwa kuwa wakazi wa eneo hilo husumbuliwa sana na magonjwa sugu kama vile UKIMWI, Kifua Kikuu, Kuhara na kadhalika.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza vyumba katika kituo hicho cha Afya ili wananchi hao waondokane na adha ya kufuata huduma hiyo kwenye hospitali za rufaa *KCMC* umbali wa km. 100 na zaidi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII (K.n.y. WAZIRI MKUU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dorah Heriel Mushi, Viti Maalum, linalohusu uhaba wa vyumba vya wagonjwa katika kituo cha Afya Mererani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010 Serikali kupitia mpango wa maendeleo wa Afya ya msingi ( MMAM) ilitenga jumla ya shilingi 145,802,000 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro na kati ya fedha hizo kituo cha Afya Mererani kilitengewa shilingi 45,624,200 kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya kina mama pamoja na chumba cha kuhifadhia maiti. Kwa mwaka 2010/2011 katika mpango wa maendeleo wa Afya ya msingi Serikali imetenga kiasi cha shilingi 100,930,000 kwa ajili ya Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro ambapo shilingi 20,000.000 zitatumika kwa ajili ya kuongeza wodi kwa ajili ya kituo cha Afya Mererani.

Mheshimiwa Spika, jitihada hizi za serikali za kuboresha huduma katika kituo cha Afya Mererani ni endelevu, ili kuweza kukabiliana na Idadi kubwa ya wakazi katika mji mdogo wa Mererani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dorah Mushi swali la nyongeza.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini kama alivyoeleza ni kwamba bado chumba cha akina mama cha kujifungulia hakijawa tayari lakini pia kutokana na umbali wa kutoka Mereani kwenda hospitali ya Rufaa inapotokea dharura bado kituo hiki kina shida ya kupatiwa usafiri kwa ajili ya akina mama wajawazito. Je, Serikali ina mpango gani wa kuweza kutoa usafiri kwa ajili ya akina mama hawa ili wasiendelee kujifungulia barabarani ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII (K.n.y. WAZIRI MKUU**): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dorah Mushi kama ifuatavyo. Kuhusu suala la usafiri Mererani nina kubaliana kabisa kwa umbali wa kilomita 50 alizozitaja ni mbali sana kiasi kwamba inaweza ikaleta tatizo kwa akina mama ambao watahitaji kujifungua hasa kwa njia ya *operation*, ninachoweza kusema ni kwamba pamoja na kuwapatia usafiri wa kuweza kupeleka wagonjwa katika hospitali kuu lakini bado tutaendelea na mapango wetu wa Afya ya msingi ambao katika *programme* yetu tutatengeneza wodi za kufanyia upasuaji katika vituo husika.

Mheshimiwa Spika, hivyo napenda niseme kwamba kadri fedha zinatapokuwa zinatutosheleza basi tutawezesha kituo hiki kiweze kutoa huduma hizi. Lakini wakati huohuo pia TAMISEMI watakuwa wanafanya mipango kama gari litapatikana kama litakavyopatikana kwa Mheshimiwa Bukwimba basi na Mheshimiwa Dorah naye anaweza akapatiwa.

**SPIKA:** Sasa ni zamu ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, ndilo swali linalofuata.

Na. 3

**Kujenga Chuo cha Michezo Mbalimbali Nchini**.

**MHE. VUAI ABDALLA KHAMIS (K.n.y. AME PANDU AME)** aliuliza:-

Serikali imefanikiwa kujenga kiwanja kikubwa na kizuri cha Mpira wa Miguu Jijini Dar es salaam.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Chuo cha Michezo mbalimbali hapa nchini?

(b) Je, Serikali imejipanga vipi kukarabati viwanja vya michezo vilivyopo Mikoani hususan kwenye Jiji la Mbeya, Tanga, Dodoma, Arusha na Mwanza ili vikidhi haja ya viwanja vya michezo vya kimataifa?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa idhini yako na kwa heshima zote ninaomba kabla sijajibu swali hili uniruhusu nitoe pongezi kwa timu yetu ya *Twiga Stars* ya akina mama kwa kuweza kufuzu kuingia fainali ya mashindano ya *Africa* kule *South Africa* mwezi *September, 2010.* Lakini pia naomba uniruhusu niipongeze timu yetu ya vijana chini ya miaka 17 kwa kipigo inachokiendeleza kule *South Africa* kwa kuishinda timu ya Botswana kwa magoli 15 kwa 2. Lakini pia uniruhusu pamoja na kuwa tumefungwa goli tano kwa moja lakini pia niipongeze timu yetu ya Taifa. Kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mbunge wa Nungwi, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali tayari ina chuo cha Michezo mbalimbali nchini ambacho kimejengwa Malya Mkoani Mwanza. Hata hivyo Serikali ina kusudia kujenga vyuo vingine endapo hali ya fedha itakuwa nzuri hapo baadaye. Kwa kutambua uwepo wa wa chuo cha Malya Serikali Serikali inaendelea na uboreshaji wa miuondombinu yake ili kiweze kuhudumia wanachuo wengi zaidi kwa pamoja. Aidha Serikali inaendelea kuhamasisha wadau mbalimbali wa michezo kuanzisha vyuo au mafunzo yanayohusiana na masuala ya michezo ili kuendeleza taaluma katika fani ya michezo katika nchi yetu.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inaona umuhimu wa kuvikarabati viwanja vya michezo vilivyopo Mikoani kama alivyotolea mfano Mheshimiwa Mbunge katika Mikoa ya Mbeya,Tanga, Arusha,Tanga, Dodoma na Mwanza ili viweze kufikia viwango vya kimataifa. Hata hivyo ikumbukwe kwamba viwanja vilivyopo katika Mikoa hiyo ambayo Mheshimiwa Mbunge amevitaja vinamilikiwa na Taasisi mbalimbali hapa nchini. Wizara yangu kwa kutumia wataalamu wake imekuwa ikifuatilia kwa karibu ili kuona kwamba vinapewa matunzo mazuri kwa ajili ya mashindan mbalimbali kama vile ya ligu kuu ya *VODACOM* na mengine yanayoandaliwa na vyama vya michezo mbalimbali nchini katika ngazi ya Mkoa na Wilaya.

Aidha Serikali imekuwa ikitoa ushauri wa mara kwa mara kwa wamiliki wa viwanja hivyo ili waweze kuingia ubia katika kumiliki viwanja hivyo baada ya kuona kuwa uwezo wa kuvitunza na kuvisimamia ni mdogo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii pia kuzikumbusha Halmashauri za Miji, Manispaa na Wilaya kuwa, moja ya vitega uchumi ambavyo vinaweza kuongeza mapato hivi sasa ni viwanja vya michezo, hivyo ni wajibu wao kutambua hilo na kuanza kulifanyia kazi ikiwa ni sehemu ya miradi ambayo itawaongezea kipato na pia kuongeza nafasi ya ajira kwenye maeneo yao. (*Makofi*)

**MHE. VUAI ABDALLA KHAMIS:** Mheshimiwa Spika ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Je, Wizara ina mpango gani kwa wachezaji bora wa timu hizo?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, ni mawazo mazuri na kwamba vyama vyote vya michezo nchini tumeviagiza kupitia Baraza la Michezo kwamba wachezaji wote bora katika nchi wawe na utaratibu wa kuwa na orodha yao na tumewaelekeza kwamba angalau kila mwaka tuwatambue na pia kuwe na tuzo ambazo wanapata ili angalau iwe ni kumbukumbu ya maisha yao.

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza napenda nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, mwaka 2007 niliuliza swali la matengenezo ya viwanja kwa kuweka nyasi bandia katika viwanja hivyo na Serikali ikanijibu kwamba haina mpango wala haina utaratibu huo kutokana na ardhi yetu kwamba ni nzuri hawawezi kuweka nyasi za bandia, baadaye kitendo hicho kimefanyika.

Serikali haioni ni vema kutangaza rasmi kwamba nyasi bandia ni nzuri na tuweze kuzitumia?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Soud amezungumzia suala la kiutalaam zaidi, katika dunia viwanja vingi ni vya nyasi za asili na ndivyo ambavyo vinafaa zaidi kuchezea na ndivyo vinavyotumika zaidi. Hata viwanja vya *South Africa* kwa bahati nzuri mimi ni Makamu Mwenyekiti wa Mawaziri wa Michezo katika Afrika ambaye nimehusika kukagua viwanja vyote kule *South Africa*, viwanja vile vyote ni vya nyasi za asili.

Mheshimiwa Spika, viwanja hivi vya nyasi bandia hatuvitumii sana kwa sababu kwanza vinasababisha wachezaji kupata matatizo wakati wanacheza wakati mwingi kwa sababu kuna viatu maalum, na hivi viwanja kwa sababu ni aghali sisi tunapata msaada, tumepata msaada wa viwanja vitatu tu, Uwanja wa Taifa, Uwanja wa Karume na Uwanja Gombani. Pindi Serikali itakapokuwa na uwezo vile viwanja ambavyo vinatumika sana tutaweza kuweka nyasi bandia.

Mheshimiwa Spika, ninashauri kwamba ni vizuri tukawa tunatunza viwanja vyetu vya nyasi za asili kwa sababu ndivyo vinavyotumika zaidi dunia. (*Makofi*)

Na. 4

**Kuondolewa kwa kipindi cha Mazungumzo baada ya Habari Radio Tanzania**

**MHE. RAJABU HAMAD JUMA** aliuliza:-

Kipindi cha mazungumzo baada ya habari za Redio Tanzania kilisaidia sana nchi yetu kushinda vita ya Kagera kwa njia ya kufanikisha uhamasishaji wa masuala mbalimbali ya maendeleo ya nchi yetu:-

(a) Je, kwa nini kipindi hicho hakisikiki tena kwa sasa kwenye redio Tanzania *(TBC)?*

(b) Je, ni mafanikio gani yaliyotarajiwa kwa kukifuta kipindi hicho?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rajabu Hamad Juma, Mbunge wa Tumbatu, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kipindi cha mazungumzo baada ya Habari kilichokuwa kikirushwa kupitia Radio Tanzania wakati huo kilisaidia sana nchi yetu kushinda vita vya Kagera kwa njia ya kufanikisha uhamasishaji wa masuala ya maendeleo ya nchi yetu. Kipindi cha mazungumzo baada ya habari kilianzishwa kutokana na ushauri wa viongozi wa chama cha *TANU* wakati huo na Mwandishi wa kwanza kabisa wa mazungumzo hayo alikuwa Mheshimiwa Paul Sozigwa ambaye amewahi kuwa Mwandishi Mkuu wa Rais, Mkurugenzi wa Redio Tanzania na Afisa Mkuu wa *TANU* na CCM.

Umaarufu wa kipindi cha mazungumzo baada ya habari ulianza kupungua pale ambapo Mheshimiwa Paul Sozigwa alipokabiliwa na majukumu mengine ya kitaifa na jitihada zilizofanywa na waandishi wengine ili kipindi hicho kiweze kuendelea zilikwama baada ya kukosa mvuto na hatimaye kupotea kabisa. Ndipo uamuzi wa kukifuta kabisa ulifuata.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umaarufu wa kipindi hicho, hususani umuhimu wake katika jamii, hivi sasa majadiliano yameanza ili kutaka kukirejesha kwenye idhaa ya Taifa ya *TBC*. Huenda kisiwe kama ilivyokuwa kwenye miaka ya 70 na 80 lakini nia ni kiwe na mvuto na msisimko wa hali ya siku hizi. Hivyo, maandalizi makubwa yanahitajika kufanywa ili kuhakikisha kwamba mazungumzo baada ya habari mapya nayo yanapata mvuto kama yale ya zamani.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishaeleza sababu za kukifuta kipindi cha mazungumzo baada ya habari, hazikuwa na malengo yeyote bali ni kutokana na kukosekana kwa mwandishi maalum ambaye angekuwa na ubunifu na fikra ambazo zingekuwa na ujumbe ambao ungekuwa na mvuto kwa wasilikizaji. Katika mazingira hayo huwezi kutarajia mafanikio yeyote kwa kufuta kipindi hicho.

**MHE. MOHAMMED HABIB MNYAA:** Mheshimiwa Spika nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, kipindi hicho kilitoweka kutokana na majukumu mengi ya Mtayarishaji wa Kipindi hicho Ndugu Sozigwa, na kwa kuwa wapo watu wenye vipaji mbalimbali nchini na muda wote Serikali ilikaa bila ya kuwatafuta mpaka imekuja suala hili ndiyo Serikali inatafakari kuanzisha tena.

Je Serikali itakuwa na mpango gani sasa ya kuwatafuta watu wenye vipaji kama hao ambao Kisiwani Pemba wapo wengi sana wenye vipaji kama hivyo mpaka vya kuimba albadiri?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye ndiyo maana Serikali inajipanga upya. Kwa hiyo, mawazo yake tunayachukua na kama wapo tunawakaribisha ofisini kwetu ili angalau tuweze kupata wabunifu kwa sababu kipindi hiki zaidi ni ubunifu. Kwa hiyo tunakaribisha mawazo hayo.(*Makofi*)

Na. 5

**Mabehewa ya Treni katika kituo kidogo cha Mbalizi**

**MHE. MCH. LUCKSON MWANJALE** aliuliza:-

Katika ajali ya treni iliyotokea miaka miwili iliyopita imeacha mabehewa ya treni hiyo yakiwa yamerundikana katika kituo kidogo cha Mbalizi na kuwa kero kubwa kwa wananchi wa maeneo hayo kwa sababu yamesababisha maficho ya vibaka na vijana wavuta bangi.

Je, ni lini mabehewa hayo yataondolewa?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Mbunge ya kwamba katika ajali ya treni iliyotokea tarehe 2 Julai, 2008 katika eneo la Mbalizi, Mkoani Mbeya, *TAZARA* ilipoteza mabehewa 37 yaliyotumbukia katika korongo baada ya kupitiliza katika sehemu iliyokusudiwa (*refuge siding.*)

Katika utaratibu wa kawaida ajali inapotokea, utafiti wa chanzo cha ajali hufanyika na baadaye matengenezo ya reli husika hufanywa ikifuatiwa na uondoshwaji wa mabehewa na vichwa vya treni katika eneo la hatari.

Mheshimiwa Spika, katika zoezi la kuyaondoa mabehewa yaliyotumbukia korongoni kutokana na ajali hiyo, kreni(*rescue crane*) moja kati ya mbili zilizokuwa

zikitumika kwa ajili hiyo ilishindwa na kuharibika vibaya jambo lililosababisha kazi kushindikana kuendelea.

Kazi ya kuanza tena kuondoa mabehewa hayo ilisimama kwa ajili ya kusubiri matengenezo ya kreni mbili kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, matengenezo ya kreni hizo hivi sasa yamekamilika na ni matarajio yangu ya kwamba kazi ya kuondoa mabehewa itaanza tena wakati wowote na inatarajiwa iwe imekamilika ifikapo mwishoni mwa mwezi Julai, 2010.

**MHE. MCH. LUCKSON MWANJALE:** Mheshimiwa Spika, nasimama kuishukuru Serikali kwa jibu zuri ahsante. *(Makofi)*

Na. 6

**Daraja la Mto Ruhekei-Mbamba Bay.**

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA** aliuliza:-

Daraja la Mto *Ruhekei-Mbamba Bay* linavunjika kila mara nyakati za masika na kusababisha kero kubwa kwa wananchi wanaosafiri kupitia njia hiyo.

Je, ni lini Serikali itajenga daraja la kudumu katika mto huo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kapteni John Damiano Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaifahamu kero kubwa ya wananchi wanaosafiri kupitia daraja la Mto *Ruhekei- Mbamba Bay* ambalo huvunjika mara kwa mara hasa nyakati za masika kama alivyoeleza Mbunge.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua kero hiyo imeandaa mpango wa kulijenga daraja hilo ili kuwaondolea tatizo la usafiri wananchi wanaotumia njia hiyo. Hivi sasa Serikali imekamilisha usanifu wa kina wa daraja hilo na Zabuni za ujenzi wa daraja hili zimefunguliwa tarehe 4 Juni 2010. Ujenzi wa daraja hili unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2010/2011. UJenzi utagharamiwa kwa pamoja na fedha za mradi wa matengenezo ya dharura zilizotolewa na Benki ya Dunia na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru Serikali kwa kutuondolea kero hii ambayo ilikuwa inaniletea mchezo mchafu Jimboni, lakini pamoja na hayo nina swali moja la nyongeza.

Kujengwa kwa daraja hili kutaendana sambamba na ujenzi wa barabara ya Mbinga/Mbamba Bay kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru kwa shukrani alizozitoa kwa Serikali ambayo inamwondolea kero kule Jimboni na sisi tunamtakia kila la kheri katika mchakato unaokuja. Lakini la pili kwamba pengine baada ya kutengeneza daraja hili uwepo pia mpango wa kutengeneza barabara kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi Serikali ina mpango mkubwa wa kuunganisha barabara zote nchini ngazi ya mikoa kwa kiwango cha lami itakapofika mwaka 2018 na baada ya hapo barabara ya ngazi zingine zitafuata.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi tunaendelea na mpango huo tutakapokuwa tumepata uwezo wa kifedha barabara hiyo nayo itafikiriwa.

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, suala lililotokea huko Mbinga linafanana kabisa na huko kwangu Kilwa Kaskazini katika Mto Matandu ulioko Njinjo, kuna Kata ambayo imekuwa kisiwa, Kata ya Kandawale hakupitiki kabisa kwa sababu ya mto Matandu.

Je, Serikali haina mpango wowote kuipatia pesa ili daraja la mto Matandu na watu waweze kwenda Kandawale kiurahisi?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Serikali niwape pole wananchi wa eneo hilo ambao sasa hivi wanapata kero hiyo ya kutokuwepo kwa daraja na kwa hiyo hawavuki kwa urahisi lakini niseme tu kwamba Bunge tunamkaribisha atuletee maelezo rasmi na sisi tuweze kuangalia utaratibu kama tulivyofanya kwa Mheshimiwa Komba.

Na. 7

**Wanaojiita Jamhuri ya Ukombozi**

**MHE. ANIA SAID CHAUREMBO** aliuliza:-

Hivi karibuni vyombo vya habari vimeripoti juu ya uvamizi wa msitu mmoja mkoani Tabora ukihusisha watu zaidi ya mia mbili (200) wenye asili ya Burundi na Tanzania waliopiga kambi msituni humo na kupeperusha bendera nyekundu na kujitangaza kama Jamhuri ya Ukombozi.

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya jambo hili?

(b) Je, Warundi na Watanzania hao wana lengo gani juu ya kutangaza Jamhuri ya Ukombozi na kupeperusha Bendera Nyekundu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mbunge wa viti maalum, lenye sehemu (a), (b) na ( c ) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Serikali ni kwamba hakuna ukweli wowote juu ya habari za watu wenye asili ya Tanzania na Burundi kupiga kambi misituni, kupeperusha bendera nyekundu au kujitangazia Jamhuri ya Ukombozi.

Mheshimiwa Spika, ukweli wa jambo hili ni kwamba wapo wafugaji kutoka Tabora na Shinyanga walivamia na kuishi na mifugo yao ndani ya msitu wa hifadhi ya mto Igombe (*Igombe River Forest Reserve).* Wavamizi wote hao ni Watanzania na hakuna raia kutoka nchi jirani ya Burundi.

Mheshimiwa Spika, tarehe 11 Mei, 2010 ilifanyika operesheni maalum ya kuwaondoa wavamizi hao ambapo watuhumiwa 28 walikamatwa ikiwa ni pamoja na ng'ombe 283, mbuzi 29 na kondoo 9. Vitu vingine vilivyokamatwa ni pamoja na bunduki 6 aina ya gobore, mtambo mmoja wa kutengenezea magobore na baruti.

Mheshimiwa Spika, zoezi la kuwaondoa wavamizi hao linaendelea na waliokamatwa wamechukuliwa hatua za kisheria zikiwemo kushitakiwa Mahakamani.

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa, taarifa hii ya uvamizi uliofanyika Tabora kati ya Watanzania na Warundi na kupeperusha bendera nyekundu na kuweka bango la Jamhuri ya Ukombozi ilitoka katika baadhi ya vyombo vya Habari, na watanzania mara nyingi wanapata habari katika vyombo hivi vya habari;

Je, Serikali itachukua hatua gani sasa kwa vyombo vya habari ambavyo vimetoa tamko hili ambalo si la ukweli badala ya kusema ni tamko ambalo lilikuwa la wafugaji?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, hiyo taarifa anayoisema ambayo ilitoka katika vyombo vya habari nikiri kwamba mimi mwenyewe binafsi sikuiona, lakini sina shaka Mheshimiwa Mbunge atakuwa anasema kitu ambacho ana ushahidi ana uhakika nacho.

Lakini pia tumekuwa tunatoa tahadhari Waziri mwenye dhamana ya vyombo hivi, Waziri mwenye dhamana ya vyombo hivi vya Habari na Wizara wamekuwa wanazungumza na vyombo hivi kuhusu utoaji wa habari na hasa kitu ambacho kimekuwa

kinazungumzwa ni ile *professionalism*, weledi wa kazi ambayo wanaifanya na kuwa na uhakika wa taarifa ambazo wanazitoa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, sasa vipi vyombo vya habari vinaweza vikapotosha ama vikaweka kitu kama hicho kwa kweli sijui, na haiwezekani na wala haiingii akilini niseme tu kwa kumjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba nchi yetu ni makini. Jeshi letu ni imara, vyombo vyetu vya ulinzi vipo sawasawa, haiwezi ikatokea eti kundi lije liingie katika Taifa letu limege sehemu ya Taifa, liseme kwamba hiyo imekuwa ni sehemu ya nchi tofauti haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, hicho kwanza ni kitu ambacho kwa kweli kinatia aibu kama kweli kimetangazwa namna hiyo. Serikali itachunguza ni vyombo gani hivyo ambavyo vilitangaza taarifa hiyo, halafu pia tutaangalia nini kinaweza kikafanyika. Nakushukuru sana Mheshimiwa Mbunge.

Na. 8

**Makato ya T.sh 5000/= kwa ajili ya Mfuko wa Huduma za Jamii**

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA** aliuliza:-

Ziko taarifa kwamba, kila askari katika Jeshi la Polisi hukatwa sh. 5000/= kila mwezi kwa ajili ya Mfuko wa Huduma za Jamii na kwamba Jeshi hilo lina askari wasiopungua 30,000.

Je, Serikali inaweza kuwaelekeza Watanzania sababu za msingi za makato hayo na huduma zipi za jamii zinazohusika na hayo makato?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mamb ya Ndani ya Nchi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitoa huduma mbalimbali kwa Askari Polisi walio kazini. Huduma hizo ni pamoja na matibabu na kugharamia mazishi na kugharamia mazishi na kutoa jeneza/ubao, sanda na usafiri hadi mahali marehemu atakapozikwa.

Aidha, Serikali ipo katika mandalizi rasmi ya kuwaingiza askari katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya hivyo huduma za matibabu kwa askari zitaboreka zaidi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kwa upande wa mazishi huduma inayotolewa kwa askari imeonekana kutotosheleza kwani inamhudumia askari peke yake na wala sio watoto na wazazi wake au wa mkewe/mumewe wanapofariki. Aidha, huduma za mazishi anazopewa askari hukoma tu mara anapostaafu.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua hali hiyo kwa kipindi kirefu (zaidi ya miaka 25 ) askari katika Mikoa au Komandi mbalimbali wamekuwa na mifuko inayojulikana kwa jina maarufu la mifuko ya "kufa na kuzikana" ambapo huchangishana fedha kila mwisho wa mwezi kwa ajili ya kusaidiana wakati wa misiba. Baada ya kufanya tathmini Jeshi la Polisi limeona kwamba mifuko hiyo imekuwa na matatizo.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa matatizo hayo Jeshi la Polisi limeufanya mfuko huo uwe wa kitaifa mfuko ambao umeanzishwa sasa uwe na wanachama wote kwa kupata huduma popote wanapofanyia kazi na hata baada ya kustaafu.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Jeshi la Polisi linao watumishi 32,381 na kila mwanachama wa mfuko atahitajika kuchangia Tshs. 5,000/= kila mwezi. Mfuko huu ni wa hiari na unatokana na maoni ya askari wenyewe na wale ambao hawataki kujiunga hawalazimishwi kuchangia.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika Jeshi la Polisi iko sheria ambayo inahusika na mazishi kwa askari pale ambapo anafariki. Na kwa kuwa sheria hii hivi sasa haikidhi kwa sababu ni sheria ya tangiaq ukoloni.

(a)Je, Serikali haioni kwamba iko haja ya kurekebisha sheria hii ili kuweza kuwasaidia hawa askari polisi kuliko kuleta utaratibu huu wa makato ya kifedha?

(b) Kwa kuwa wako baadhi yao hawana watoto au familia. Je, watu kama hawa sheria inawachukuliaje hawa ambao hata ukoo wao hawana?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba taratibu nyingi katika Jeshi la Polisi hazijachukuliwa hatua, hazijatazamwa tangu wakati wa Ukoloni. Hiyo ni sahihi na ndio maana sasa hivi Wizara inalo zoezi la maboresho. Maboresho haya yanachukulia masuala yote ambayo yanahusu Jeshi la Polisi hapa nchini. Yatakuwa ni maboresho ya kipindi cha miaka kumi na shughuli hii imefikia mbali na kuna waraka tayari umepelekwa katika Baraza la Mawaziri. Ni jambo ambalo linajadiliwa na kutazama ni vipi tunaweza tukaboresha maslahi ya wafanyakazi hawa muhimu kwa taifa letu.

Lakini suala la kukatwa kama nilivyosema katika jibu langu la msingi Mheshimiwa Mbunge siyo suala la lazima ni suala la hiari. Wale ambao watakubaliana na hilo basi wanachangia mchango wao. Wale ambao hawakubaliani nalo hawalazimishwi wala hawatakatwa fedha zao. *(Makofi)*

Kuhusu swali la pili la Mheshimiwa Mbunge wale ambao hawana familia au hawana watoto ni kweli polisi wengi wanapoanza kazi wanakuwa bado ni vijana wanakuwa bado hawana familia. Lakini hii tunazungumzia utaratibu ambao atakuwa nao Polisi katika miaka trakriban 30 au 35 au 40 ambao atakuwa anafanyakazi katika Jeshi la Polisi.

Nahisi wengi katika kipindi hicho watakuwa wamepata familia au watakuwa nadhani watakuwa wamepata familia. Kwa hiyo, katika kukujibu nisijibu nadharia lakini nadhani ukweli ni kwamba waliokuwa wengi baada ya kufanya kazi kwa muda mrefu wanakuwa na familia na niseme kwamba Mfuko huu ambao tunauweka kwa kweli utakuwa ni mfuko wa manufaa na utaweza kuwasaidia. Ni kama vile unavyoona mimi na wewe na wengine huko ambao wanakuwa na mikataba katika mifuko mbalimbali iwe ni mifuko ya *pension,* au mifuko ya matibabu na kadhalika.

Na. 9

**Chanjo ya ugonjwa wa midomo na Miguu kwa ng'ombe**

**MHE. GOSBERT B. BLANDES** aliuliza:-

Ugonjwa wa midomo na miguu ya ng'ombe umekuwa ukijirudiarudia hapa nchini, na pengine kwa sababu ya chanjo ya ugonjwa huo ni ghali sana kiasi kwamba wafugaji wengi hushindwa kuilipia.

Je, Serikali haitoi ruzuku ya chanjo hiyo kwa wafugaji?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mbunge wa Karagwe, naomba kutoa maelezo yafuatayo.

Kuanzia mwaka 2005/2006 Serikali ilianza utaratibu wa kutoa ruzuku kwa madawa na chanjo ya magonjwa hatari yanayosababisha vifo vingi vya mifugo. Magonjwa hayo ni pamoja na Ndigama kali, Homa ya Mapafu ya Ng'ombe, Homa ya Bonde la Ufa na Ugonjwa wa Sotoka ya Mbuzi na Kondoo. Katika kipindi cha mwaka 2005/2006 hadi mwaka 2009/2010 fedha za ruzuku zilizotolewa ni shilingi bilioni 21.53 kama ifuatavyo:-

(i) Shilingi bilioni 13.5 kwa ajili ya dawa za kuogeshea mifugo, ambapo ng'ombe milioni 15.5 waliogeshwa;

(ii) Shilingi bilioni 1.8 kwa ajili ya chanjo ya Homa ya Mapafu, ambapo ng'ombe milioni 11.4 walichanjwa;

(iii) Shilingi bilioni 6.0 kwa ajili ya chanjo ya Homa ya Bonde la Ufa, ambapo ng'ombe millioni 2.9, mbuzi milioni 1.4 na kondoo 600,000 walichanjwa; na

(iv) Shilingi milioni 232.8 kwa ajili ya chanjo ya Sotoka na mbuzi na kondoo ambapo mbuzi na kondoo milioni 3.6 walichanjwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo ni kweli kuwa Ugonjwa wa Miguu na Midomo si wa hatari ikilinganishwa na magonjwa ya milipuko niliyotaja hapo juu na kutokana na ufinyu wa Bajeti ya Serikali, chanjo ya ugonjwa huu haijaanza kutolewa ruzuku.

Hata hivyo, kadri bajeti ya Serikali itakaavyoimarika chanjo ya kudhibiti ugonjwa wa Miguu na Midomo nayo itaapatiwa ruzuku. *(Makofi)*

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri hapa amesema kwamba ugonjwa huu si wa hatari ikilinganishwa na magonjwa mengine ya mlipuko nilitaka kumwuliza Mheshimiwa Waziri kama anafahamu kwamba ugonjwa huu husababisha vifo vingi vya mifugo na pia ng'ombe wengi wenye mimba huweza kuharibu mimba.

(a) Je, hilo analifahamu?

(b) Kwa kuwa chanjo hii mpaka sasa hivi haipatikani hapa nchini ni chanjo ambayo inapatikana kutoka nchi za nje ikiwemo Kenya na nchi zingine. Sasa ni kwa nini chanjo hii haitengenezwi hapa nchini ili kuweza kupunguza gharama za chanjo na kuwapunguzia adha kubwa sana wafungaji? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ugonjwa wa midomo na miguu huwa unasababisha vifo vya mifugo. Lakini ukilinganisha hatari yake ilivyo mfano ukiangalia ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa ulipotokea vifo vingi sana vilitokea hata binadamu aliathirika.

Lakini ugonjwa wa midomo na miguu unapotokea maafa yake huwa siyo makubwa na huweza kudhitiwa. Mfano katika mwaka 2009/2010 ng'ombe karibu 2000 waliathirika lakini ng'ombe waliokufa walikuwa watano (5) tu.

Kwa hiyo, kutokana na hali hiyo huwa tunaona kwamba unaweza kudhibitiwa na wafugaji wenyewe.

Kuhusu swali la pili, kwamba kwa nini chanjo hii haitengenezwi hapa nyumbani? Tunayo maabara pale Temeke ambayo hutengeneza chanjo mbalimbali lakini ni zile ambazo tuna utalaam na vifaa. Kwa hiyo, kutokana na ugonjwa wa miguu na midomo bado chanjo yake hatujaweza kuitengeneza lakini maabara hii inaboreshwa ili tuweze kutoa chanjo hii nayo pia.

**MHE. MICHAEL LEKULE LAIZER:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mwaka jana mifugo walikufa kwa wingi sana na wafugaji kuwa maskini.

Je, Serikali itachukua utaratibu gani kuwasaidia hawa wafugaji hata kuwapa dawa bure au wachangie nusu kwa vile hawana uwezo wa kununua madawa ya mifugo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tunafahamu kwamba kutokana na ukame uliotokea mifugo mingi sana ilikufa sehemu za Kaskazini mwa Tanzania na hali ya wafugaji tunaifahamu.

Labda kama nilivyosema katika swali langu la msingi yale magonjwa ya mlipuko ambayo ni hatari Serikali itaendelea kuyatolea ruzuku ili mifugo isiathirike zaidi. Vile vile kama tutangalia hali ugonjwa wowote utakapotokea na tukaangalia kwamba hali ni mbaya mno Serikali haitasita kuchukua hatua ili kuwanusuru wafugaji. *(Makofi)*

Na. 10

**Chanjo ya Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwaa**

**MHE. OSCAR R. MUKASA** aliuliza:-

Katika majibu ya swali la nyongeza kwa swali na 111 lililoulizwa kwenye mkutano wa 19 ni kwamba hapa nchini wapo mbwa 4,000,000 na mpaka sasa Serikali inaweza kusambaza dozi 50,000 za dawa za chanjo ambapo dozi moja inaweza kutumika kwa mbwa 10 na hivyo dozi zilizopo zinaweza kufikia 13% ya malengo ya chanjo kitaifa ambayo ni 65% katika kutokomeza tatizo hili nchini:

(a) Je, Serikali inaweza kutoa taarifa ya jitihada zinazoendelea ili kutoa chanjo kufikia kiwango kinachostahili?

(b) Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuwezesha kutambua mbwa aliyechanjwa ili wananchi waweze kushiriki katika kuwatambua wale mbwa ambao hawajapata chanjo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu**:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, Mbunge wa Biharamulo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mheshimiwa Spika, kutokana na Mkakati wa kudhibiti Ugonjwa wa kichaa cha Mbwa, Wizara yangu imekuwa ikitoa chanjo za kichaa cha mbwa na kuzisambaza kwenye Halmashauri kwa ajili ya kuchanja mbwa katika maeneo yao. Kuanzia 2005/2006 hadi 2009/2010, jumla ya chanjo/dozi 550,000 zilinunuliwa na kuchanja mbwa 500,000.

Aidha, kuanzia mwaka 2009/2010 kupitia mradi wa kudhibiti na kutokomeza kichaa cha mbwa unaosimamiwa na Shirika la Afya Ulimwenguni (*WHO*), chini ya ufadhili wa Taasisi ya *Bill and Melinda Gates*, Serikali imeanza kutekeleza mpango wa kuchanja mbwa 400,000 kwa kipindi cha miaka mitano (5). Katika mwaka 2009/2010 chanjo dozi 99,000 zimenunuliwa na kusambazwa kwenye Halmashauri 24 zenye matukio mengi ya ugonjwa huu. Pia, magari manne na pikipiki 17 zimenunuliwa kwa ajili ya kutekeleza mradi huu. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, ili kutambua mbwa waliochanjwa, Serikali imekuwa inawapatia vyeti vya chanjo wafugaji wa mbwa. Vyeti hivyo huonyesha tarehe ya chanjo na kituo ambacho chanjo imetolewa. Ili kuboresha utambuzi wa mbwa waliochanjwa, Serikali imenunua mishipi ya shingoni *(dog collars)* 12,000 na kuanzia sasa mbwa akichanjwa atawekewa mshipi shingoni ili iwe rahisi kutambua mbwa aliyechanjwa. Utaratibu huu unatekelezwa chini ya sheria ya magonjwa ya mifugo na 17 ya mwaka 2003, kifungu Namba 46.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru majibu ya Naibu Waziri pamoja na kwamba naomba marekebisho ya jina ni Mukasa siyo Mutasa.

(a) Kwa kuwa tatizo la kichaa cha mbwa linazidi kuwa kubwa kwenye maeneo mbalimbali hapa nchini ikiwemo Kata za Nyakahula, Nakalenge Wilayani Biharamulo na kwa kuwa majibu ya Wizara yanadhihirisha upungufu mkubwa kwenye kazi tunayoifanya sasa katika hilo kwa sababu tunachanja si zaidi ya asilimia 15 ukilinganisha na asilimia 65 inayotakiwa kimataifa kwa *standard* za kimataifa ili kukabiliana na tatizo hili.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza nguvu zaidi kwa maana ya fedha na rasilimali zingine ili kutokomeza shida hii kwa sababu ufinyu wa Bajeti haukutajwa kama sehemu ya tatizo hii ndogo tunayoifanya?

(b) Je, Serikali iko tayari kuwashirikisha wamiliki wa mbwa hawa katika kuchangia gharama za kuchanja mbwa wao ili tuongeze wigo tuweze kukaribia zaidi hiyo asilimia 65, kiwango ambacho ni kiwango cha kimataifa? Nashukuru.

**SPIKA:** Kabla Mheshimiwa Naibu Waziri hujajibu, Mheshimiwa Mukasa unafuga mbwa au? Ahsante sana, endelea.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ni kweli kwamba Bajeti huwa ni matatizo lakini tunajitahidi sana kuhakikisha kwamba kichaa cha mbwa kinapotokea tumekidhibiti kwa sababu huu ni ugonjwa hatari. Mtu akiumwa akipata ugonjwa wa kichaa cha mbwa huwa hali yake ni mbaya sana.

Kwa hiyo, nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba unapotokea tu ugonjwa tunadhibiti na ndiyo maana kwa sasa hivi tumepata ufadhili kutoka *Bill and Melinda Gates* ambao wametupatia fedha na vifaa kwa ajili ya kuchanja mbwa laki nne kwa mwaka.

Lakini kama hali itatokea mbaya na ikaonekana kwamba Bajeti hiyo fedha haitoshi, Serikali haitasita kuongeza kwa sababu haiwezi kuachia watu wake wanakufa na kichaa cha mbwa. Kuhusu kwamba Serikali ishirikiane na wananchi na wananchi nao walipie ugonjwa huu ni hatari sana Serikali itajitahidi kwa namna yoyote inavyoweza kuweza kudhibiti ugonjwa huu.

Lakini basi kama utatokea kwa bahati mbaya na Serikali haijafika na dozi ipo siyo kosa mwananchi akanunue hiyo dozi na kuweza kumtibu mbwa wake. Lakini nia ni kuhakikisha kwamba ugonjwa huu wa hatari unadhibitiwa kutokana na Serikali yenyewe, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kasi ya kuchanja mbwa haiendani na idadi ya mbwa waliopo na madhara yatokanayo na mbwa ambao hawakuchanjwa husababisha maradhi kutokana na kichaa cha mbwa. Tiba ya maradhi hayo ni kubwa sana na wanaoathirika ni wananchi wengi kule vijijini ambao kipato chao ni kidogo sana.

Je, sasa Serikali ina mpango gani wa kutoa tiba ya bure kwa wahanga wote ambao watapatikana na matatizo ya kuumwa na mbwa wenye kichaa?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ugonjwa huu ni hatari sana. Kwa kweli nimewahi kuona mtu ameumwa na mbwa, hali yake huwa mbaya sana, na utamwonea huruma. Sasa nia hasa ni kuzuia lakini ninavyoamini katika hospitali kama mwathirika na kuumwa na mbwa wa kichaa, akiumwa hali ile ambayo huwa anayo sidhani kama hospitali zetu zitamwacha afe kwamba hana hela.

Naamini kwamba tutajitahidi pale ambapo hali ni mbaya wagonjwa hao kuweza kutibiwa bure mpaka hapo anapopona na aweze kulipa ama kusamehewa kutokana na hali ilivyo. Ugonjwa huu ni hatari sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maelezo ya nyongeza kwamba chanjo ya kichaa cha mbwa inatolewa bure haina gharama yoyote kwa mhanga. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii. Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha na muda wa kusitisha kipindi cha maswali umefika. Matangazo ni kama ifuatavyo. Kwanza wageni.

Waheshimiwa Wabunge wa Majimbo ya Manyoni Mashariki na Magharibi, ambao ni Mheshimiwa John Chiligati Waziri wa Nyumba na Maendeleo ya Makazi na wa Mashariki, Mheshimiwa John P. Lwanji Mbunge wa Manyoni Magharibi, wanao wageni wao ambao ni Makatibu Kata wa Chama cha Mapinduzi kutoka Wilaya ya Manyoni wakiongozwa na Katibu wa CCM wa Wilaya hiyo Ndugu Mathias Shidagisha. Naomba wasimame pale walipo tuwatambue. Ahsanteni sana.

Karibuni sana Bungeni na nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenu kwa kutumia hekima kuwaleta ili muangalie mambo yalivyo. Basi mnajua majibu tena mtasaidiana huko huko jimboni. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, saa tano leo asubuhi kutakuwa na Kikao muhimu sana cha Kamati ya Uongozi kuzungumza na Serikali kuhusu mwelekeo wa Bajeti. Wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi mnaombwa kuhudhuria bila kukosa Ukumbi wa Pius Msekwa, siyo Ukumbi wa Spika ni Ukumbi wa Pius Msekwa, saa tano leo asubuhi, Kamati ya Uongozi kwa mashauriano na Serikali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, leo saa nane mchana kutafanyika kikao chetu cha *briefing* na saa kumi itakuwa ni ile mikutano ya kawaida ya makundi ya vyama vya siasa. Wabunge wanakutana kwa mujibu wa Kanuni katika makundi yao ya vyama vya siasa.

Huo ndiyo mwisho wa matangazo. Kwa kuwa shughuli zilizopangwa leo zimeisha basi naahirisha Bunge hadi hapo saa tatu asubuhi kesho.

*(Saa 4.05 Asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano,*
*Tarehe 9 Juni, 2010 Saa Tatu Asubuhi)*